

"MATATIZO YA UKALIMANI: UCHAMBUZI

WA MAHUBIRI YA KIDINI"

NA

LOGONDA, JOSEPHINE EMILY ADUDA

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA
BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA
YA 'MASTER OF ARTS' KATIKA CHUO
KIKUU CHA NAIROBI.

University of NAIROBI Library



0472637 8

AUGUST

1998.

UNGAMO

"Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe
na haijatolewa kutosheleza mahitaji
ya shahada katika Chuo Kikuu
kingine chochote."

EA

JOSEPHINE E.A OGONDA

(Mtahiniwa)

"Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa
idhini yetu tukiwa wasimamizi wa
kazi hii wa Chuo Kikuu."

BI. ROSE SHAKE

Mj. J. Njuguna

BI. MARGARET NJUGUNA

TABARUKU

Namtabarukia tasnifu hii baba
yangu,

BW. AMBROSE OPIYO OGONDA

Kwa kugharamia masomo yangu.

YALIYOMO

YALIYOMO	(i)
SHUKURANI	(iii)
MUHTASARI	(iv)

SURA YA KWANZA

1.0	UTANGULIZI	1
1.1	SOMO LA U'AFITI	2
1.2	MADHUMUNI YA TASNIFU	2
1.3	SABABU ZA KUCHAGUA SOMO HILI	3
1.4	YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI	3
1.5	UPEO WA TASNIFU	6
1.6	HAIPOTHESIA	6
1.7	MSINGI WA KINADHARIA	6
1.8	NJIA ZA U'AFITI	7
	TANBIHI	10

SURA YA PILI

2.0	UTANGULIZI	11
2.1	MASIALA YA UKALIMANI	11
2.2	TAFSIRI NA UKALIMANI	14
2.3	AINA ZA UKALIMANI	18
	2.3.1 UKALIMANI WA KUFUATISHA	19
	2.3.2 UKALIMANI SAWIA	20
	TANBIHI	22

SURA YA TATU

3.0	UTANGULIZI	23
3.1	MATATIZO YA KIISIMU	23

3.1.1	KIWANGO CHA KIFONOLOJIA NA KIFONETIKI ..	23
3.1.2	KIWANGO CHA SINTAKSIA	28
3.1.3	KIWANGO CHA KILEKSIA	32
3.1.4	KIWANGO CHA MAANA	37
	TANBIHI	42

SURA YA NNE

4.0	UTANGULIZI	43
4.1	MATATIZO MENGINE YASIYO YA KIISIMU	43
4.1.1	MAFUNZO KWA WAKALIMANI	43
4.1.2	UJUMBE MREFU	46
4.1.3	HISIA ZA MKALIMANI	49
4.1.4	SAIKOLOJIA YA MKALIMANI	51
	TANBIHI	55

SURA YA TANO

5.0	HITIMISHO NA MAPENDEKEZO	56
	MAREJELEO	59

SHUKURANI

Natoa shukurani zangu za dhati kwa wasimamizi wa kazi hii Bi. Rose Shake na Bi. Margaret Njuguna kwa ushauri wao ulioniongoza katika kuandika kazi hii.

Shukurani zangu vilevile ni kwa wahadhiri wafuatao; Dkt. Kithaka wa Mberia, Dkt. Gideon Marete, Bw. Zachary Mosoti, Bw. Mwenda Mbatia, Bw. Leonard Muaka, Dkt. Kineene wa Mutiso na Bw. Gichobi Mungania kutoka Idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Nairobi. Pia namshukuru kwa dhati Bw. Daudi Chacha wa Chuo Kikuu cha Egerton kwa kunipa misingi dhabiti katika somo la tafsiri pamoja na Bw. Muindi na Bw. Issa Mwamzandi.

Siwezi kuwasahau wanafunzi wenzangu Leah Muchemi, Florence Omusula, Bella Kiteki, Phillip Ochoi, Solomon Khaemba, Hezron Mogambi, Jonathan Muga, Timothy Arege na Gideon Kiptanui tulioshirikiana nao darasani na hata nje ya darasa.

Nawapa wazazi wangu Bw. Ambrose Opiyo na Bi. Mary Opiyo shukurani zangu za moyo na hasa baba kwa bidii yake katika kunielimisha.

Shukurani za kipekee pia ni kwa Arnold na Foxie Wekesa kwa kunipa moyo na ari ya kuendelea na kazi hii nilipokuwa karibu kukata tamaa.

Shukurani pia ni kwa wakalimani ambao hawakutaka kutajwa kwa majina kwa kunisaidia katika utafiti wangu.

Mwisho namshukuru Charity kwa kupiga chapa kazi hii.

MUHTASARI

Tasnifu hii inashughulikia matatizo ya ukalimani ambapo kwa kuchambua mahubiri ya kidini, tumeweza kuyabainisha baadhi ya matatizo hayo. Kazi yenyewe imegawanywa katika sura tano.

Sura ya kwanza ni utangulizi. Katika utangulizi wa sura hii tumeweza kutoa maelezo mafupi kuhusu historia ya ukalimani. Tumezungumzia pia kuhusu somo la utafiti, madhumuni ya tasnifu na haipotesia zilizotungoza katika utafiti wetu. Zaidi ya hayo tumeweza kuangalia yaliyoandikwa kuhusu somo hili ambapo tuliweza kupitia kazi zilizoandikwa kuhusu tafsiri na ukalimani. Vilevile tumeweza kutoa sababu zetu za kuchagua somo hili, msingi wa kinadharia na upeo wa tasnifu. Hatimaye tumeweza kueleza njia tulizotumia katika utafiti wetu.

Sura ya pili inazungumzia masiala mbalimbali kuhusiana na ukalimani. Katika sura hii tumeweza kuangalia dhana ya ukalimani na kuilinganisha na tafsiri. Kwa kufanya hivyo tumeweza kuona tofauti na ushabihiano ulioko kati ya dhana hizi mbili. Mwisho tumeangalia aina mbalimbali za ukalimani.

Sura ya tatu inahusu uchambuzi halisi wa data tuliyokusanya. Katika sura hii tumezingatia matatizo ya kiisimu katika viwango vinne: fonolojia, sintaksia, leksia na maana. Tumetoa mifano kuonyesha vile makosa yanavyojitokeza katika kila kiwango.

Sura ya nne inashughulikia matatizo yasiyo ya kiisimu.

Hapa tumejaribu kuoanisha matatizo haya na yale ya kiisumu ili kuona vile matatizo yasiyo ya kiisumu yanavyoweza kuchangia yale ya kiisumu.

Sura ya tano ni hitimisho. Katika sura hii tumetoa maelezo ya kijumla kuhusu utafiti wetu na matokeo yake. Pamoja na hayo, tumetoa mapendekezo.

ALAMA ZILIZOTUMIKA:

UA - UJUMBE ASILIA

UT - UJUMBE ULIO'AFSIRIWA

Mtsh - MATAMSHI

Mndsh - MAANDISHI

... (faded text) ...

... (faded text) ...

... (faded text) ...

... (faded text) ...

... (faded text) ...

... (faded text) ...

... (faded text) ...

1.0 UTANGULIZI

Tafsiri ya Bibilia inaweza kuorodheshwa kati ya tafsiri za awali zaidi. Tafsiri hizi zilifanywa na wageni - hasa wamishonari¹ ambao walikuja Bara la Afrika kueneza neno la Mungu.

Sambamba na tafsiri za Bibilia kulikuwa na haja ya kufasiri mahubiri hasa kutokana na sababu kuwa Waafrika wengi hawakuelewa lugha ya Kiingereza ambayo ilitumiwa na wamishonari.

Ukalimani wakati huu ulikuwa na matatizo mengi kwa sababu wakalimani waliotumiwa kufasiri hawakuwa na weledi wa kutosha katika lugha ya Kiingereza. Wengi walikuwa wamejifunza lugha hii kijuujuu bila kupitia taratibu yoyote ya masomo.

Kumekuwa na ripoti zisizoweza kuthibitishwa² kuwa, ukalimani wakati huo hasa ulitumika kuwachekesha waafrika ambao walichukuliwa na wazungu kuwa mazuzu. Ndiposa kumezuka mizaha kuhusu taaluma hii ya ukalimani. Kwa mfano,

UA: Jesus will come back.

UT: Yesu alikuwa Mkamba.

UA: Halleluya

UT: Alikuwa Mluyia

UA: As I was preaching in Johannesburg.

UT: Nilipokuwa nahubiri huko mfuko wa Yohana...

Ufasiri wa aina hii unaonyesha vile kunaweza kuwa na upotoshaji wa ujumbe iwapo mizaha itaingizwa katika taaluma hii.

Katika siku za hivi karibuni tunaweza kusema kuwa

kiwango cha ukalimani ni cha juu kwa kiasi fulani ingawa bado kuna matatizo ya hapa na pale. Hii hasa inatokana na sababu kuwa wakalimani wengi wanao ujuzi wa lugha mbili zinazohusika: Kiswahili na Kiingereza Chambilecho Nida (1947: 96)

"Mtafsiri lazima awe anafahamu vilivyo lugha zote mbili: lugha asilia na lugha pokezi".

(tafsiri yetu)

1.1. SOMO LA UTAFITI

Katika kazi hii tumeangalia matatizo yanayozuia uwasilishaji wa ujumbe katika ufasiri wa mahubiri ya kidini. Tatizo kubwa katika aina hii ya tafsiri ni kuwa hii ni tafsiri ya papo kwa hapo hivyo muda wa kufikiria ni mdogo. Kutokana na jambo hili ujumbe asilia unaweza kupotoshwa.

Kama Nida (1947:86) anavyosema,

"Hakuna tafsiri ambayo hufanywa mara moja na kuwa kamilifu bila kuwa na haja ya kuipitia tena".

(Tafsiri yetu)

Tunakubaliana na maoni ya Nida kuwa kudurusu tafsiri ni hatua muhimu katika kufikia tafsiri ya kiwango cha juu.

Hivyo tatizo linalomkumba mkalimani ni kuwa hana fursa ya kupitia ujumbe aliofasiri na kurekebisha makosa ambayo huenda aliyafanya.

1.2 MADHUMUNI YA TASNIFU

Tumeangalia dosari zinazojitokeza katika mahubiri ya kidini tuliyoyachagua. Kwa kuchunguza dosari hizi tumeweza kugundua kiini cha matatizo hayo.

Tumechunguza na kuonyesha vile udhaifu wa ufasiri katika mahubiri ya kidini, unavyoweza kuwa kikwazo katika uwasilishaji wa ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa.

Tumejaribu kutathmini dosari ambazo mkalimani anaweza kuziepuka na zile ambazo haziwezi kuepukika.

Ni matumaini yetu kuwa mapendekezo tuliyoyatoa yataweza kuboresha zaidi mahubiri ya kidini yaliyotafsiriwa pamoja na kazi zingine za ukalimani.

1.3 SABABU ZA KUCHAGUA SOMO HILI

Ukalimani ni muhimu katika mahubiri ya kidini kwani huwezesha ujumbe kuwafikia watu wengi zaidi. Utafiti wetu hivyo unakusudia kuangalia matatizo yanayoweza kuwa kikwazo katika kufanikisha lengo hili.

Ingawa mengi yameandikwa kuhusu tafsiri tawi la ukalimani halijashughulikiwa vilivyo hasa tukizingatia kuwa tafsiri kama hii huwasilishwa katika lugha zungumzi wala si andishi kama ilivyo katika tafsiri za aina nyingi.

Kazi yetu imeangalia mifano halisi ya kazi za ukalimani na kuainisha matatizo yanayowakabili wakalimani. Kwa kufanya hivyo ni matumaini yetu kuwa tumetoa mchango katika tawi hili la ukalimani.

Taaluma hii ya ukalimani katika mahubiri ya kidini imekuwa kama kaida hivi kwamba lengo lake hasa la kupitisha ujumbe huwa balizingatiwi. Hivyo kazi nyingi za ukalimani hufanywa bila makini.

1.4 YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI

Kazi za Nida (1947, 1964) zimetufaa sana kwani ameshughulikia kwa undani tafsiri ya Bibilia. Anazungumzia kwa urefu kaida mbalimbali za kutafsiri pamoja na mikondo ambayo kazi ya tafsiri sharti ipitie. Ufafanuzi wake kuhusu umuhimu wa kupata mafunzo kwa wale wanaotarajia kufanya kazi ya tafsiri umetuwezesha kuangalia kwa undani vile ukosefu wa mafunzo unavyoweza kuwa tatizo kwa

mkalimani.

Achilles (1967) anamulika baadhi ya matatizo katika tafsiri. Ingawa anashughulikia lugha za Kiingereza na Kichina nasi tumeshughulikia Kiingereza na Kiswahili, matatizo anayotaja hasa kuhusu umuhimu wa kuzimudu vilivyo lugha mbili zinazohusika umetufaa katika utafiti wetu.

Fuller (1984) ameshughulikia elementi ambazo hufanya tafsiri kuwa nzuri. Anashughulikia tafsiri katika mikutano ya kimataifa akitumia lugha za Kifaransa, Kihispania na Kiingereza. Anakiri kuwa ingawa amefanya kazi hii kwa muda mrefu, yeye hukumbana na matatizo mara kwa mara. Anasisitiza umuhimu wa kujiandaa kabla ya kuanza kazi ya ukalimani. Kutokana na utafiti wetu tumeona umuhimu wa kujiandaa kama suluhisho la baadhi ya matatizo yanayoweza kumkabili mkalimani.

Glemet (1958) ameshughulikia matatizo ya ukalimani katika mikutano ya kimataifa. Anaendelea kueleza matatizo yanayoweza kumkabili mkalimani katika ukalimani wa kufuatisha na ukalimani sawia. Maelezo yake kuhusu ukalimani wa kufuatisha yametufaa sana katika kazi yetu kwani ndio unahusika katika mahubiri ya kidini tuliyoyashughulikia.

Ali (1981) anajadili makosa mbalimbali yanayojitokeza katika taarifa za habari zilizotafsiriwa kutoka Kiingereza hadi Kiswahili katika Sauti ya Kenya. Sisi tumeangalia matatizo ya ukalimani katika mahubiri ya kidini ambayo huwasilishwa katika lugha zungumzi. Hata hivyo baadhi ya makosa anayojadili yanajitokeza pia katika kazi ya ukalimani.

Zaja (1986) ameshughulikia fasihi tafsiri katika ukuzaji wa fasihi ya Kiswahili akimulika matatizo na athari zake juu ya fasihi kwa ujumla.

Amejikita katika kazi moja ya fasihi tafsiri ya Wema Hawajazaliwa. Sisi hatukushughulikia tafsiri ya vitabu vya fasihi.

Shitemi (1990) amezungumzia kuhusu uteuzi wa mtafsiri ili kuhakikisha kuna mawasiliano katika kazi zilizotafsiriwa. Uteuzi huu, anavyosema utategemea mtu binafsi kwani mtu mwingine anaweza kuwa na uteuzi ulio tofauti. Anatutahadharisha kuwa tofauti katika uteuzi haufai kuchukuliwa kama makosa anayofanya mtafsiri. Huu umekuwa mwongozo mzuri tulipokuwa tunachambua tafsiri ya mahubiri ya kidini.

Omondi (1997) anachunguza matatizo ya aina mbalimbali yanayotokana na kusesitizwa kwa dhana za maana na mawasiliano katika tafsiri. Katika kazi yetu tumetumia nadharia ya tafsiri maana na ile ya tafsiri mawasiliano. Hivyo ufafanuzi wake wa dhana hizi mbili zimetufaa.

Mutie (1997) anaangalia matatizo ya kuhamisha sanaa katika kazi zilizotafsiriwa, kwa kurejelea tamthilia ya Mizigo. Ni maoni yake kuwa sanaa hudhoofika katika kazi zilizotafsiriwa hasa kwa upande wa fani. Hili ni tatizo ambalo aghalabu hujitokeza katika kazi yoyote ile ya tafsiri. Katika kazi yetu tumeweza kugundua kuwa kazi iliyotafsiriwa kwa kiwango fulani hukosa mguso ulioko katika kazi asilia.

Namulungu (1997) anaangalia ukiushi kama mojawapo ya mbinu zinazotumiwa katika tafsiri kwa kurejelea Shamba la Wanyama. Maoni yake ni kuwa wakati mwingi mwandishi wa tafsiri hulazimika kutumia mbinu hii. Katika kazi yetu tumekumbana na mifano ambapo mkalimani anakiuka mambo fulani katika ujumbe asilia. Hivyo maelezo yake kuhusu ukiushi katika kazi ya tafsiri yametuwzesha kutambua ukiushi katika kazi tulizoshughulikia.

Kazi hii imeshughulikia ufasiri wa mahubiri ya kidini.

Katika kazi yetu tumeshughulikia madhehebu matatu kupata data tuliyotumia. Tumeainisha tafsiri ya mahubiri kutoka makanisa matatu jijini Nairobi ambayo ni:

- 1) Deliverance Church - City Centre.
- 2) S.D.A Church - Jericho.
- 3) Kenya Assemblies of God - BuruBuru.

Katika kila mojawapo ya makanisa tumechagua kipindi kimoja kila Jumapili au Jumamosi kwa majuma matatu. Uteuzi huu utatupa data mwafaka katika utafiti wetu.

1.6 HAIPOTHESIA

1. Sentensi katika ujumbe asilia unapokuwa mrefu sana, mkalimani anaweza kupata tatizo la kutafsiri.
2. Makosa yanayofanywa na mhubiri wa ujumbe asilia humulikwa katika fasiri.

1.7 MSINGI WA KINADHARIA

Kulingana na Newmark (1988) lengo kuu la kazi yoyote ya tafsiri ni kuwasilisha ujumbe. Kulingana na ukweli huu tumetumia nadharia ya tafsiri mawasiliano ambayo hujaribu kutoa tafsiri kama ilivyo katika lugha asilia na katika kiwango cha lugha ambacho kitaeleweka na wapokeaji ujumbe. Mtafsiri huwa na uhuru wa kiasi fulani kubuni yale anayoyawasilisha hivyo si lazima atumie maneno yale yaliyotumiwa katika lugha asilia.

Tumechagua nadharia hii hasa kutokana na sababu kuwa inazingatia vipengele muhimu ili kutathmini mawasiliano katika kazi zilizotafsiriwa. Vipengele hivi ni kama vile maneno, sarufi, wakati, muktadha, hadhira na mazingira. Na kama tujuavyo ujumbe hueleweka vyema kupitia mfumo wa kisarufi, kimaana na kisintaksia wa lugha pokezi. Hivyo

nadharia hii inaelekea kujumlisha mambo mengi yanayotoa tafsiri bora.

Tumetumia pia nadharia ya tafsiri maana kama nadharia changizi kwani nadharia hii huenda sambamba na ile ya mawasiliano. Asemavyo Zaja (1986:45)

"Katika wakati fulani, tafsiri maana na tafsiri mawasiliano hupatana na kutiliana nguvu..."

Katika nadharia hii maana huhamishwa vivyo hivyo kutoka lugha asilia hadi lugha pokezi bila kubadilisha jambo lolote.

Larson (1984:32) anasisitiza umuhimu wa maana ili kuhakikisha kuwa kuna mawasiliano. Anasema kuwa;

"Maana inayochaguliwa huathiriwa na hali ya mawasiliano. Kwa mfano itategemea msemaji ni nani, hadhira inayohusika na utamaduni wa jamii husika. Msemaji hutegemea hali ya mawasiliano ili kuchagua jambo analotaka kuwasilisha".

(Tafsiri yetu)

Hivyo nadharia hii imetoa mchango katika kuhakikisha kuwa maana iliyo katika lugha asilia inawasilishwa katika lugha pokezi bila kuathirika kwa maana hiyo.

1.8 NJIA ZA UTAFITI

Tumesoma kazi za kinadharia kuhusu taaluma ya tafsiri na ukalimani maktabani. Nadharia hizi zimetupa mwongozo katika utafiti wetu.

Tumerekodi mahubiri na kuyatumia kama data kuonyesha makosa yanayojitokeza katika ufasiri. Data hii imekusanywa bila kuwajulisha wakalimani wanaohusika nia yetu hasa ya kurekodi mahubiri hayo. Aidha, wakati mwingine tuliweza kunukuu sisi wenyewe makosa yaliyojitokeza katika ufasiri.

Tumewahoji wakalimani ili kutambua baadhi ya matatizo wanayokumbana nayo katika kazi yao. Kwa ujumla tuliweza kuwahoji wakalimani 10, wanawake wawili na wanaume wanane.

Tumetumia hojaji ili kupata maoni mengi zaidi kutoka kwa wakalimani ambao hatungeweza kuwahoji ana kwa ana.

Hojaji hizo ziligawanywa katika makanisa mbali mbali.

Jumla ya hojaji 20 ziliweza kusambazwa na hatimaye tukaweza kukusanya hojaji 13 ambazo wakalimani waliweza kuyajibu maswali tuliyowauliza.

KIJALIZO

- S1: Kwa ufupi ukalimani ulianza vipi?
- S2: Lengo hasa la ukalimani ni nini?
- S3: Je, kwa maoni yako lengo hili limefanikiwa? Eleza.
- S4: Je, umepata mafunzo yoyote kuhusu kazi hii? Eleza.
- S5: Una maoni gani kwa ujumla kuhusu kazi hii ya ukalimani?
- S6: Ni matatizo gani unayokumbana nayo katika kazi hii?
- S7: Je, wewe hufanya matayarisho ya aina gani kabla ya kuanza kazi hii?
- S8: Kuna malipo yoyote unayopata kutokana na kazi hii?

TANBIHI

1. Dr. Steere anasifika sana kwa kazi aliyofanya ya kutafsiri sehemu ya Biblia na vitabu vya maombi.
2. Maoni ya baadhi ya wakalimani.

Maoni ya baadhi ya wakalimani...

Maoni ya baadhi ya wakalimani...

MAONI YA OMBIJI

Maoni ya baadhi ya wakalimani...

Maoni ya baadhi ya wakalimani...

(Maoni ya baadhi ya wakalimani)

Maoni ya baadhi ya wakalimani...

Maoni ya baadhi ya wakalimani...

Maoni ya baadhi ya wakalimani...

2.0 UTANGULIZI

Katika sehemu hii tumeangalia dhana ya ukalimani kulingana na wataalamu mbalimbali wa lugha.

Ingawa sio nia yetu kuingilia kwa undani dhana ya tafsiri tumeonelea ni bora kulinganisha tafsiri na ukalimani ili tuweze kuona tofauti na ushabihiano kati ya dhana hizi mbili.

Mwisho tumeonelea ni muhimu kuzibainisha aina mbalimbali za ukalimani na vile zinatumika, pamoja na baadhi ya matatizo yanayoweza kumkabili mkalimani katika kazi yake anapotumia aina hizi za ukalimani.

2.1 MASIALA YA UKALIMANI

Ukalimani ni taaluma ambayo haijashughulikiwa sana hasa ikilinganishwa na tafsiri. Asemavyo Smith (1958:VII) katika dibaji ya Aspects of Translations;

"Ukalimani katika mikutano ya
kimataifa ni uwanja mgeni
kwa uchunguzi wa Kisayansi"

(tafsiri yetu)

Ndiposa hata ni nadra kupata kamusi inayoelezea ukalimani moja kwa moja.

Maelezo mengi tuliyoyotoa kuhusiana na ukalimani yanatokana na nomino mkalimani. Kutokana na utafiti wetu tuligundua kuwa hakuna maelezo ya neno ukalimani hasa katika kamusi za kiswahili¹. Hivyo imetubidi kutumia neno mkalimani kuelezea neno ukalimani.

Glemet (1958: 105) hata hivyo anatambua umuhimu wa ukalimani. Anatoa mfano wa mkutano wa kimataifa unaojumuisha wawakilishi kutoka sehemu mbalimbali wanaozungumza lugha tofauti. Katika kikao kama hiki,

anaendelea kusema, kutakuwa na haja ya kutumia wakalimani kuhakikisha kuwa ujumbe unapitishwa kwa wawakilishi wote. Hivyo huduma ya wakalimani huwa muhimu.

Pamoja na hayo tuligundua kuwa baadhi ya maelezo yanayotolewa kuhusu tafsiri na ukalimani yanafanana hivi kwamba yaelekea kuwa dhana hizi mbili zinachukuliwa kumaanisha jambo moja. Kwa mfano katika Kamusu ya Kiswahili Sanifu (1981:172) mkalimani inaelezwa kuwa,

"mtu afasiriye lugha moja
kwa nyingine".

Hivyo kutokana na maelezo haya tunaweza kueleza ukalimani kama kufasiri lugha moja kwa nyingine². Maelezo haya hayatofautishi tafsiri na ukalimani, kwani kamusi hiyo hiyo inaeleza tafsiri kama "mawazo yaliyotolewa kutoka lugha moja hadi nyingine".

Katika Longman Dictionary of Contemporary English (1987:552), ukalimani unaelezwa kuwa,

"kuweka maneno yaliyozungumzwa
katika lugha moja hadi
lugha nyingine"

(tafsiri yetu)

Maelezo haya yanatuelekeza zaidi kwa upande wa tafsiri ya neno kwa neno.

Iwapo tutazingatia maelezo haya tutaegemea katika tafsiri ya moja kwa moja ambayo wakati mwingi hupotosha ujumbe uliokusudiwa. Na kama asemavyo Zaja (1986:37),

"Tafsiri za moja kwa moja husisitiza maafikiano katika tafsiri ya neno kwa neno, maana kwa maana na umbo kwa umbo. Kwa usemi mwingine tafsiri hizi husisitiza kufikishwa kwa kile kilichoko katika makala inayotafsiriwa katika lugha pokezi kama kilivyo katika lugha ya makala".

Hivyo ni maoni yetu kuwa maelezo hayo kuhusu ukalimani yanaweza kuwa potovu.

A Dictionary of Linguistics (1969:103) inaeleza mkalimani kuwa,

"mtu anayeelezea maana ya
kitu - hasa anayetafsiri kwa
njia ya mdomo kutoka lugha
moja hadi nyingine".

(tafsiri yetu)

Hivyo tunaweza kuelezea ukalimani kama kuelezea maana ya kitu kwa njia ya mdomo kutoka lugha moja hadi nyingine³. Maelezo haya yanatupa mwelekeo zaidi kwani yanasisitiza umuhimu wa maana katika tafsiri. Licha ya hayo yanatofautisha tafsiri na ukalimani - ukalimani unarejelea tafsiri kwa njia ya mdomo.

Katika Dictionary of Language and Linguistics (1972:116) ukalimani unaelezwa kuwa,

"tafsiri inayofanywa kwa njia
ya mdomo na mtu aliye na
umilisi wa lugha zote mbili
zinazohusika pamoja na mada
inayohusika".

(tafsiri yetu)

Maelezo haya yanasisitiza umilisi wa lugha na mada inayohusika mambo ambayo ni muhimu katika tafsiri yoyote ile.

Katika Kamusi ya Isimu na Lugha
(1990:23) ukalimani unaelezwa kuwa,

"tendo la kuhamisha habari
iliyo katika lugha moja na
kuiweka katika lugha nyingine
kwa kusema".

Maelezo haya ni hafifu kwani kuna mengi yanayotokea katika ukalimani mbali na kuhamisha habari kama inavyoelezwa. Ni maoni yetu kuwa iwapo tutachukulia kuwa ukalimani ni tendo la kuhamisha habari, yaelekea hili ni tendo lililofanywa bila kufuata utaratibu wowote. Tendo kama hili linakosa usanii ambao ni muhimu katika kazi ya tafsiri.

Kutokana na maelezo tuliyotoa hapo juu, ukalimani kwa ufupi unaweza kuelezwa kama tafsiri inayotolewa na mtu aliye na umilisi wa lugha mbili zinazohusika, pamoja na mada inayohusika, kwa njia ya mdomo⁴.

2.2 TAFSIRI NA UKALIMANI

Tafsiri na ukalimani ni mambo yanayokamilishana. Kulingana na Glemet (1958:119) wazo kuwa ukalimani na tafsiri ni mambo ambayo hayawezi kupatanishwa ni la kupotosha. Jambo hili linadhihirika kutokana na ushabihiano ulioko kati ya ukalimani na tafsiri. Anaendelea kusema kuwa mkalimani huangalia vitu kupitia darubini ya kutazama mbali ilhali mtafsiri hutumia darubini ya kutazamia vitu vidogo sana. Hapa anajaribu kuonyesha kuwa ingawa jinsi ya kufanya kazi hizi mbili ni tofauti, mambo haya mawili yanachangiana katika kuleta faida fulani.

Kutokana na maelezo mbalimbali yaliyotolewa na wataalamu mbalimbali wa lugha kuhusu dhana hizi, tofauti kubwa inayodhihirika ni kuwa ukalimani hutolewa kwa njia ya mdomo⁵. Kutokana na tofauti katika uwasilishaji wa kazi ya tafsiri na ile ya ukalimani tunaona kuwa tafsiri huweza kuhifadhika kwa muda mrefu tofauti na kazi ya ukalimani ambayo huhifadhika katika akili. Kazi ya ukalimani huweza kuhifadhika kwa muda mrefu iwapo itanaswa katika kanda, jambo ambalo ni nadra kutokea. Pia kuna hatari ya kurekodi mambo yasiyohitajika. Kwa mfano katika utafiti wetu tulikumbana na tatizo hili ambapo kelele za kusukumwa kwa viti kanisani zilinaswa katika mahubiri tuliyorekodi.

Katika tafsiri, mwandishi hujiieleza kupitia maneno hivyo inambidi atafute maneno yanayoafiki anachotaka kusema.

Kwa upande wa ukalimani mbali na maneno kuna matumizi ya ishara za mwili pale ambapo mkalimani anahisi hajajieleza vizuri kwa kutumia maneno. Hutokea wakati mwingine ambapo mkalimani huambatanisha maneno pamoja na ishara za mwili. Kwa mfano kama anazungumzia kutembea , mbali na kutaja neno hilo atalifanya tendo lenyewe la kutembea. Kama anakubaliana na jambo fulani huenda akatingisha kichwa anaposema neno ndiyo. Hivyo ishara hizi huweza kufidia kwa kiwango fulani upungufu unaoweza kujitokeza mkalimani anapofasiri ujumbe fulani. Mwandishi anayetafsiri huwa hana nafasi ya kutumia ishara hizi.

Mwandishi wa tafsiri anaweza kupitia yale aliyoyatafsiri na kurekebisha makosa aliyoyafanya kabla ya kuwasilisha kazi yake kwa msomaji wake. Mkalimani kwa upande mwingine hana muda mrefu wa kufikiria yale anayohitajika kufasiri hivyo huwa na wakati mgumu kwani anakabiliana na hadhira yake papo hapo. Hivyo hana wakati wa kurekebisha makosa anayofanya. Ndiposa Brown (1983:5) anasema kuwa,

"Mwandishi anaweza kuyapitia yale aliyoyaandika, akaangalia kila neno alilotumia bila ya hofu ya kusumbuliwa na msomaji wake, anaweza kuchukua wakati wake kuchagua kila neno analotumia, hata aangalie katika kamusi na kubadilisha nia ya kile alichotaka kusema".

(tafsiri yetu)

Katika tafsiri, mwandishi huwa hana nafasi ya kupata hisia za wasomaji wake kuhusu kazi yake kama ni ya kuridhisha au la. Mkalimani kwa upande wake huweza kuonana ana kwa ana na hadhira yake hivyo anaweza kutambua hisia za hadhira kutokana na mapokezi ya ujumbe anaotoa.

Kwa upande wa umbo, sentensi zinazotumiwa na mkalimani

huwa nyingi hazijakamilika kwani matamshi yake hujitokeza kama vipande vya vishazi. Mwandishi wa tafsiri kwa upande wake lazima atumie sentensi zilizokamilika na kutumia uakifishi kwa njia inayofaa. Jambo hili huwa muhimu kuhakikisha kuwa anachokitafsiri kinaeleweka na wasomaji wake.

Mkalimani huwa anasikizwa na hadhira yake. Hivyo sauti ni chombo muhimu katika kuhakikisha kuwa yale anayosema yanapokelewa na wasikilizaji wake. Iwapo sauti ya mkalimani itakuwa ya chini basi anayosema hayatapokelewa vyema na hadhira yake. Jambo hili laweza kuwa tatizo hasaiwapo hakuna chombo cha kupaza sauti. Sauti anayotumia mkalimani pia ni muhimu katika kuibua hisia za wasikilizaji wake. Hivyo iwapo mkalimani atatumia sauti legevu basi hamu ya kusikiliza miongoni mwa waumini huenda ikawa ya chini sana. Uwezo wa mkalimani kutumia sauti inayopanda na kushuka huchangia sana katika kudumisha usikivu. Tofauti katika tafsiri si lazima mwandishi awe na kipawa cha kutumia sauti kwa ushupavu. Hii ni kutokana na sababu kuwa kile anachotafsiri kitasomwa wala si kuzikizwa na hadhira yake.

Hadhira inayolengwa na mkalimani au hata mhubiri wa ujumbe asilia inajumuisha watu kutoka viwango mbali mbali⁶. Hivyo lugha inayotumiwa sharti iwe lugha sahili itakayoeleweka moja kwa moja na waumini wengi bila matatizo. Ujumbe anaotoa yafaa uwe rahisi kushika na kueleweka. Katika tafsiri, mwandishi ana uhuru wa kutumia lugha changamano au sahili kutegemea hadhira anayolenga. Kwa mfano tafsiri iliyokusudiwa kusomwa na watoto wa shule za msingi itaandikwa kwa lugha sahili ikilinganishwa na tafsiri inayokusudiwa kusomwa na wanafunzi wa Vyuo Vikuu, kwani kiwango chao cha lugha ni cha juu zaidi, kikilinganishwa na kile cha watoto wa shule za msingi.

Katika kazi ya ukalimani, msikilizaji, tofauti na msomaji katika tafsiri hawezi kurudi nyuma na kuyapitia tena mambo fulani ambayo hakupata maana. Hivyo iwapo ujumbe fulani utampita msikilizaji hana njia nyingine ya kuupata ujumbe huo. Kwa upande wa msomaji yeye anaweza kurudi nyuma na kusoma tena yale ambayo hakuyaelewea.

Mkalimani ana muda mfupi sana kufanya kazi yake ukilinganishwa na ule wa mtafsiri. Mtafsiri ana muda wa kutafsiri na kupitia kazi hiyo na kufanya marekebisho ya hapa na pale. Mkalimani naye husikiza tu na tayari anahitajika kuupata ujumbe na kuutafsiri bila ya muda wa kutosha wa kutafakari yale anayosema.

Uwezo wa kukumbuka ni muhimu kwa mkalimani. Ni lazima atie akilini ujumbe asilia kabla hajapewa nafasi ya kutoa fasiri yake. Tofauti na mwandishi wa tafsiri ambaye ana makala asilia anayoweza kurejelea mara kwa mara bila matatizo.

Tofauti na tafsiri ambapo msomaji huwa hayapokei makala asilia na tafsiri yake wakati mmoja, katika ukalimani msikilizaji huwa na fursa ya kusikiliza ujumbe asilia na ule uliotafsiriwa kwa pamoja.

Licha ya tofauti tulizoelezea hapo juu kuna ushabihiano mkubwa kati ya ukalimani na tafsiri. Kwanza kabisa zote huhusisha makundi matatu. Katika tafsiri kuna;

- i) Mwandishi wa makala asilia
- ii) Mwandishi wa tafsiri
- iii) Msomaji

Katika ukalimani kuna;

- i) Mtoaji ujumbe asilia
- ii) Mfasiri wa ujumbe (mkalimani)
- iii) Msikilizaji

Zote huhusisha lugha mbili ambapo lugha moja inatafsiriwa hadi lugha nyingine. Tafsiri sawa na ukalimani huwa na lengo moja

ambalo ni kuwasilisha ujumbe kwa wale ambao hawaelewi lugha asilia:

Mwisho mkalimani, sawa na mtafsiri hufuata mkondo unaofuatwa na anayetoa ujumbe asilia. Mtafsiri naye atafuata mkondo uliofuatwa na mwandishi asilia. Kwa mfano iwapo mwandishi asilia wa kitabu alianza kitabu kwa kutumia mbinu rejeshi, anayetafsiri hana budi kufuata mkondo huo huo. Kwa upande wa mkalimani iwapo mhubiri asilia ataanza mahubiri yake kwa kuwasalimu waumini, mkalimani hana budi kufanya vivyo hivyo.

Ni muhimu kusema kuwa tofauti tulizobainisha katika sehemu hii (ya 2.2) zinarejelea hasa ukalimani katika mahubiri ya kidini. Kikao kama hiki huwa cha hadhara zaidi, kikilinganishwa na vikao vingine kama vile mikutano ya kimataifa ambako ukalimani hutumika.

Tofauti hizo pia zimebainishwa kwa kulinganisha lugha zungumzi na lugha andishi hivyo ni vigumu kutofautisha vile zinavyojitokeza katika mazungumzo ya anayetoa ujumbe asilia na anayetoa tafsiri. Ni kutokana na sababu hii ndipo tumeyaangalia kwa pamoja.

Ni muhimu pia kuelewa kuwa kuna muingiliano mkubwa kati ya lugha zungumzi na lugha andishi hasa pale ambapo lugha andishi inatumiwa kutayarisha kazi itakayowasilishwa katika lugha zungumzi. Katika hali kama hii lugha andishi huathiriwa na lugha zungumzi.

2.3 AINA ZA UKALIMANI

Kuna aina mbili kuu za ukalimani:

- i) Ukalimani wa kufuatisha⁷
- ii) Ukalimani sawia⁸

Kati ya aina hizi mbili za ukalimani, inayotumika katika mahubiri ya kidini ni ile ya kufuatisha.

2.3.1 UKALIMANI WA KUFUATISHA

Katika aina hii ya ukalimani, mkalimani hutoa fasiri ya ujumbe asilia katika vifungu vifupi huku anayetoa ujumbe asilia akitua mara kwa mara kumwachia nafasi mkalimani atoe fasiri yake. Crystal (1987) pia anaongezea kuwa mkalimani anaweza kutoa fasiri yake mwisho wa mahubiri.

Asemavyo Crystal (1987: 349) aina hii ya ukalimani ni wa jadi - wakati wa Mnara wa Babeli. Aina hii ya ukalimani hutumika katika mikutano midogo ya kibiashara au ya kibinafsi. Pia hutumiwa na watu wanaopokea wageni hasa watalii na kuwatembeza katika sehemu mbalimbali. Aina hii ya ukalimani ndiyo hutumika katika mahubiri ya kidini kama tulivyotaja hapo juu.

Kutafsiri ujumbe mrefu katika aina hii ya ukalimani unawezekana tu iwapo mkalimani ana uwezo wa kunukuu mambo muhimu akilini mwake. Hivyo kiwango cha ufahamu wa mkalimani huwa muhimu. Tutaeleza zaidi kuhusu tatizo hili la ujumbe mrefu katika sura ya nne (4.1.2).

Kuhusu ukalimani katika mahubiri ya kidini, mkalimani huwa hana habari kuhusu ujumbe atakaozungumzia mhubiri. Hii ni kutokana na imani ya kidini kuwa mhubiri hapaswi kuzungumza na yeyote juu ya ujumbe atakaotoa kabla ya kufika kwa saa za mahubiri. Pia kuna uwezekano wa mhubiri

kubadilisha ujumbe wake kutokana na vile atakavyoongozwa na roho mtakatifu. Kutokana na jambo hili kuna uwezekano wa kuongeza, kupunguza au kubadilisha kabisa ujumbe katika mahubiri. Kutokana na hali hii isiyokuwa na utaratibu wowote ni vigumu kwa mkalimani kujiandaa vilivyo. Hata hivyo kutokana na utafiti wetu kuna wale waliokuwa na maoni tofauti kuhusu jambo hili kama tulivyoweza kugundua kutokana na hojaji tulizosambaza.

2.3.2 UKALIMANI SAWIA

Aina hii ya ukalimani hutumika katika mikutano mikubwa hasa ya kimataifa ambapo ufasiri hufanywa kupitia vyombo vya kupaza sauti au mazungumzo kwa sauti ya chini. Wale wanaohitaji huduma za ukalimani huvaa vifaa vya masikizi ambavyo huweza kutoa tafsiri moja kwa moja.

Crystal (1978) anasema kuwa aina hii ya ukalimani ni wa hivi karibuni ikilinganishwa na ile ya kufuatisha. Anaendelea kusema kuwa aina hii ya ukalimani ni changamano zaidi hivyo huhitaji ujuzi mkubwa.

Katika aina hii ya ukalimani, mkalimani husikiza ujumbe asilia na wakati huo huo hutoa fasiri. Anayetoa ujumbe asilia huwa hapumui kumpatia fursa ya kufasiri. Msikilizaji anayetumia huduma hii ya mkalimani huweza kusikiza lugha zote mbili zinazohusika kwa pamoja. Aina hii ya ukalimani huwa ya kiwango cha juu ikilinganishwa na ile ya kufuatisha.

Katika aina hii ya ukalimani matumizi ya maneno mengi ya ziada ni jambo ambalo haliwezekani kwani mkalimani sharti afuate mwendo ulio sawasawa na ule wa mzungumzaji wa ujumbe asilia. Mkalimani huwa hana fursa ya kusikiliza ujumbe asilia kabla ya kutafsiri kwani yote huenda sambamba. Asemavyo Crystal (1978:349),

"Akili lazima ikumbuke yale
yaliyosemwa, ishughulikie
yale yanayosemwa na
kufikiria yale yatakayosemwa"

(tafsiri yetu)

Mkalimani ataelekea kutumia maneno hasa anayotumia mzungumzaji wa ujumbe asilia lakini sharti anayosema mkalimani yawe na maana, hivyo si kumaanisha atatumia tafsiri ya moja kwa moja. Baadhi ya mambo muhimu katika

aina hii ya ukalimani ni:

- i) kusikiliza kwa makini
- ii) uwezo wa kufahamu makosa na kurekebisha umbo na mfumo wa kisintaksia
- iii) kutafsiri papo kwa hapo

Kulingana na Glemet (1958), aina hii ya ukalimani wakati mwingine umejulikana kama sanaa ya kuhamisha masimulizi ya mzungumzaji kutoka kwa mdomo wa mzungumzaji hadi masikio ya mkalimani na kutoka kwa mdomo wa mkalimani hadi masikio ya msikilizaji bila kupitia akilini mwa yeyote.

Ni muhimu kwa mkalimani kuwa macho kuhusu mambo ya kisiasa na kiitifaki kwani kama tulivyosema hapo juu aina hii ya ukalimani hutumika katika mikutano mikubwa ya kimataifa ambayo hujumuisha watu kutoka nchi mbalimbali ulimwenguni. Zaidi ya hayo ni muhimu kwa mkalimani kujua mkutano unahusu nini kabla ya kuingia kwenye jumba la mkutano. Asemavyo Glemet (1958:108), jambo hili litamwezesha mkalimani kubashiri msamiati atakayokumbana nayo na kujitayarisha vilivyo na tafsiri.

TANBIHI

1. Kama vile Kamusi ya Kiswahili Sanifu (1981), Kamusi ya Kiswahili (1975) na A Standard Swahili - English Dictionary (1977).
2. Katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu (1981:172).
3. Katika A Dictionary of Linguistics (1969:103).
4. Fasili hii imefikwa kutokana na fasili mbalimbali zilizotolewa na wataalamu wa lugha kama vile Pei M.A (1969: 103) na Hartmann R.R.K. (1972:116)
5. 'Njia ya mdomo' imetumika kumaanisha ufasiri unaotolewa kwa lugha zungumzi tofauti na lugha andishi.
6. Viwango vya kutiliwa maanani ni kama vile umri, uana na kiwango cha elimu.
7. Ni fafsiri yetu ya 'consecutive interpreting' inayopatikana katika A Dictionary of Language and Linguistics (1972:116)
8. Tafsiri yetu ya 'Simultaneous interpreting' kama 7 hapo juu.
9. Neno tua limetumika kama tafsiri ya 'pause'.

SURA YA TATU

3.0 UTANGULIZI

Katika sura hii tumeangalia shida zinazomkabili mkalimani zinazotokana na matatizo ya kiisimu. Matatizo ya kiisimu hujitokeza katika viwango mbalimbali kutokana na jinsi mtu anavyotumia lugha. Tumeshughulikia viwango vya kifonolojia, kisintakisia, kileksia na kimaana.

Kwa kutoa mifano halisi tumeweza kuonyesha vile matatizo haya yanavyojitokeza katika viwango hivi vinne.

3.1 MATATIZO YA KIISIMU

3.1.1 KIWANGO CHA KIFONOLOJIA NA KIFONETIKI

Lugha hutofautiana katika kiwango cha sauti. Kuna sauti zinazopatikana katika lugha moja ambazo hazipo katika lugha nyingine.

Kama tulivyosema katika sura ya pili, kazi ya ukalimani huwasilishwa kwa kutumia lugha zungumzi. Kutokana na jambo hili, matamshi huwa muhimu kuhakikisha kuwa ujumbe unawasilishwa vilivyo. Matamshi mabaya yanaweza kusababisha upotoshaji wa maana. Matamshi mabovu hasa hutokana na athari ya lugha ya mama ambayo ni lugha ya kwanza kwa watu wengi. Catford (1969:61) anaeleza kuhusu matamshi katika kiwango cha fonolojia. Anasema,

"Tafsiri ya kifonolojia
hujitokeza kama matamshi
mabovu miongoni mwa
watu wanaozungumza lugha
ngeni.. Hii ni athari ya
kifonolojia na ni maoni yetu
kwamba inatokana na uhamishaji
wa fonolojia ya lugha ya
kwanza katika lugha ya pili."

(tafsiri yetu)

Kutokana na utafiti wetu tumegundua kuwa tatizo la
matamshi huwa kikwazo kikubwa kwa wakalimani walio na
athari ya lugha za kwanza. Kutokana na mahojiano na
baadhi ya wale walio na tatizo hili tuliweza kugundua
kuwa wengi wao huwa wanafahamu kile wanachomaanisha lakini
katika kiwango cha utendaji huwa wanapata matatizo. Ili
kuthibitisha jambo hili waliweza kutuandikia maneno
ambayo katika kiwango cha matamshi wanatamka vingine.

Mfano 1:

Mtsh: Waumini wote wanaarikwa
katika kalamu ya kumuaga
Mchungaji wetu.

Mndsh: Waumini wote wanaalikwa
katika karamu ya kumuaga
Mchungaji wetu.

Mfano 2:

Mtsh: Mpende Chirani yako
kama vile unavyochipenda

Mndsh: Mpende jirani yako kama
vile unavyojipenda.

Chomsky anatofautisha umilisi na utendaji. Cresswell
(1978:9)¹ akirejelea yale aliyosema Chomsky, anaeleza

dhana hizi mbili kama ifuatavyo;

"Umilisi ni ule ujuzi alionao
mtu kuhusu lugha yake
ilhali utendaji ni jinsi
anavyotumia ujuzi huo wa
lugha katika hali halisi
kimazungumzo na kimaandishi"

(tafsiri yetu)

Kutokana na maelezo haya tunaweza kusema kuwa tatizo alilionalo mkalimani katika kiwango cha matamshi huwa linajitokeza katika utendaji mbali si kuonyesha kuwa hana umilisi katika lugha inayohusika. Wakalimani walio na matatizo ya kimatamshi walitueleza kuwa tatizo hili linatokana na ukosefu wa mojawapo ya sauti zinazohusika katika lugha yao ya kwanza.

Kutokana na data tuliyokusanya tuliweza kupata mifano ifuatayo:

Mfano 1:

UA: They were singing in the Church.

UT: Walikuwa wanaiba Kanisani.

Tafsiri inayotolewa hapa inatoa ujumbe tofauti na ule ulioko katika ujumbe asilia. Ujumbe utapotoshwa hapa iwapo anayepokea ujumbe uliotafsiriwa haelewi lugha asilia. Tukitafsiri maana ya ujumbe tunaopata kutoka Kiswahili hadi Kiingereza tunapata ujumbe ufuatao:

They were stealing in the Church

Tafsiri iliyo sawa kimatamshi inafaa iwe:

Walikuwa wanaimba Kanisani

Mfano 2:

UA: Jesus told Simon to let down
the net for a catch.

UT: Yesu alimwambia Simoni ashushe nyavu ili
afue samaki

Afue ina maana ya kusafisha kitu kama vile nguo. Maana
iliyokusudiwa katika ujumbe asilia ni kutoa samaki majini.
Hivyo tafsiri sawa inafaa iwe;

Yesu alimwambia Simoni ashushe nyavu ili
avue samaki.

Hata hivyo kutokana na uchunguzi wetu tuliqundua kuwa
kuna wakati ambapo sauti mbili zinazoleta matatizo hubadilishana.
Kwa mfano,

UA: Every citizen has a right to vote.

UT: Ni haki ya kila mwananchi kupiga kula.

Tafsiri sahihi:

Ni haki ya kila mwananchi kupiga kura.

Kutokana na mfano huo pale ambapo mkalimani anahitajika kutia
sauti [r] anatia [U] na pale ambapo anahitajika kutia sauti
[U] anatia sauti [r].

UA: It is important to bless our food
before eating.

UT: Ni muhimu kutoa shukrani kabla ya kura.

Tafsiri sahihi:

Ni muhimu kutoa shukrani kabla ya kula.

Pia tuliweza kugundua kuwa wakalimani hupata matatizo

iwapo anayetoa ujumbe asilia ana matatizo katika matamshi yake. Kulingana na mkalimani mmoja tuliemhoji mhubiri wa ujumbe asilia anapotamka neno kwa njia isiyo sahihi, mkalimani wakati mwingine huenda akatoa tafsiri ambayo haiteti maana iliyokusudiwa.

Mfano 1:

UA: We should respect readers

UT: Tunapaswa kuwaheshimu wasomaji

Makosa yanayojitokeza hapa yanatokana na matamshi mabovu katika ujumbe asilia. Mhubiri wa ujumbe asilia alikuwa na maana ya:

We should respect leaders

ambayo tafsiri yake ingekuwa: Tunapaswa kuwaheshimu viongozi.

Tafsiri inayotolewa katika mfano huu inathibitisha haipotesia yetu ya pili kuwa baadhi ya makosa yanayotokea katika tafsiri hutokana na ujumbe asilia.

Mfano 2:

UA: Jesus raised the son of a window
in a town called Nain.

UT: Yesu alifufua mwana wa mjane
mmoja katika mji wa Naini.

Katika mfano huu, licha ya kwamba kuna matatizo ya kimatamshi katika ujumbe asilia, mkalimani anarekebisha kosa hilo katika tafsiri yake. Tunaweza kutumia mfano huu kupinga haipotesia yetu ya pili kuwa sio makosa yote yanayojitokeza katika ujumbe asilia yanamulikwa katika tafsiri.

Hapa tunaona jukumu la mkalimani kurekebisha makosa yasiyokusudiwa ambayo huenda yakafanywa na mhubiri wa ujumbe asilia. Mkalimani mmoja alitueleza kuwa tatizo hili linaweza kukabiliwa iwapo mkalimani ataelewa matatizo aliyonayo mhubiri wa ujumbe asilia kwa upande wa matamshi.

3.1.2 KIWANGO CHA SINTAKSIA

Katika kiwango hiki, tumeangalia muundo wa sentensi anazounda mkalimani na kama zinafuatana na muundo wa sentensi za Kiswahili. Katika Kiswahili, pronomino inapotumika badala ya nomino, huwa haionyeshi uana. Kwa mfano,

UA: She came yesterday

UT: Alikuja jana.

Katika tafsiri tunaona kuwa anayepokea ujumbe uliotafsiriwa hawezi kubainisha uana. Huu ni upungufu ulioko katika lugha yenyewe, hivyo mkalimani hawezi kuupekua.

Hata hivyo kutokana na utafiti wetu, tumegundua kuwa wakalimani wengi huathiriwa na muundo wa lugha ya Kiingereza, hivyo wanapotafsiri wao hutumia muundo wa Kiingereza katika Kiswahili.

Mfano 1:

UA: My dear Christians...

UT: Nyinyi Wakristo wapendwa...

Katika tafsiri hii mkalimani anatumia kielezi 'nyinyi' kama tafsiri ya 'my' katika ujumbe asilia. Muundo huu hauafikiani na muundo wa lugha ya Kiswahili. Mpangilio

bora zaidi ingekuwa:

Wakristo wapendwa...

Mfano 2:

UA: For that to happen...

UT: Kwa hilo kutendeka...

Katika mfano huu mkalimani ametafsiri moja kwa moja kutokana na muundo wa sentensi ya lugha asilia. Hata ingawa ujumbe uliokusudiwa huwafikia waumini, jambo hili hukiuka sheria za kisintaksia katika lugha ya Kiswahili.

Jambo lingine ambalo tumeangalia hapa linahusiana na upatanisho wa Kisarufi² ambalo tuligundua linatatiza wakalimani wengi na mara nyingi huwa halizingatiwi. Kutokana na utafiti wetu tumefikia uamuzi kuwa upatanisho wa kisarufi hukiukwa na watu wengi hasa katika mazungumzo. Wakalimani, ambao hutoa tafsiri kwa lugha zungumzi, vilevile hukabiliwa na tatizo hili.

Mfano 1:

UA: Something that...

UT: Kitu ambayo

badala ya

Kitu ambacho...

Mfano 2:

UA: I have seen this happen in my life.

UT: Nimeona jambo hii ikitendeka
katika maisha yangu.

badala ya:

Nimeona jambo hili likitendeka katika maisha
yangu.

Upatanisho wa kisarufi huwatatiza hasa watu ambao hawazungumzi lugha za kibantu kama lugha ya kwanza. Hii ni kutokana na sababu kuwa lugha za kibantu huwa na upatanisho wa kisarufi hivyo wanaozungumza lugha hizi huwa na uzoevu fulani wa kufuata sheria hiyo. Hata hivyo kutokana na utafiti wetu, tulipata kugundua kuwa hata wakalimani wanaozungumza lugha za kibantu hukabiliwa na tatizo hili. Mifano tuliyotoa hapo juu ni tafsiri ya wakalimani wanaozungumza Kikuyu na Kitaita kama lugha zao za kwanza. Iwapo madai haya ni kweli basi hatungetarajia matatizo kama haya. Ni bora zaidi kama tutachukulia madai haya kama kighairi wala si sheria³.

Maoni ya wakalimani ni kuwa tatizo hili linatokana na hali ya kutaka kurahisisha matamshi au kutumia lugha kama ilivyozeleka na wengi hasa katika mazungumzo. Ni maoni ya mmoja wa wakalimani kuwa binadamu kwa kawaida huwa hapendi kujichochea anapozungumza, mradi tu apitishie ujumbe. Anatupa mifano katika mazungumzo ya kila siku ambapo utamsikia mtu akisema,

1. Kichwa inaniuma.

badala ya

Kichwa kinaniuma.

2. Jina yako ni nani?

badala ya

Jina lako ni nani?

Katika uchambuzi wetu wa mahubiri yaliyotafsiriwa tulikumbana na tabia ya wakalimani kuongeza kiambishi {-nga} katika mwisho wa kitenzi cha kauli ya kuzoea. Kulingana na Mbaabu (1988)⁴, jambo hili hutokea miongoni mwa wazungumzaji wa lugha ya Kiluyia kutokana na athari ya lugha yao wanapozungumza na hata kuandika Kiswahili. Hata hivyo kutokana

na utafiti wetu tuligundua kuwa athari hii imevuka mipaka na inatumiwa na takriban watu wengi ambao hawazungumzi Kiiyua kama lugha ya kwanza.

Mfano 1:

UA: What do you think of me?

UT: Je unafikirianga nini kunihusu?

badala ya

Je, wewe hufikiria nini kunihusu?

Mfano 2:

UA: There are people who go to Church every Sunday...

UT: Kuna watu ambao huendanga Kanisani kila Jumapili...

badala ya

Kuna watu ambao huenda Kanisani kila Jumapili...

Pamoja na hayo kuna mazoea ya kuongeza kiambishi {-ko} baada ya kitenzi.

Mfano,

UA: Jesus told the Samaritan woman to give him some water to drink.

UT: Yesu alimwambiako mwanamke Msamaria ampatieko maji ya kunywa.

badala ya,

Yesu alimwambia mwanamke Msamaria ampatie maji ya kunywa

Tatizo lingine ambalo tuliweza kugundua hapa ni kuchanganya ndimi katika ukalimani.

Mfano 1:

UA: Somebody who hangs around

UT: Mtu wa kuhanghang around

badala ya,

Mtu wa kuzurura ovyo ovyo

Mfano 2:

UA: People you believed in let you down.

UT: Watu uliowaamini wamekulet down

badala ya,

Watu uliowaamini hawakufanya ulivyotarajia.

Tafsiri iliyotolewa inatumia muundo wa kufanyika kwa kitendo kwa kuongeza kiambishi {ku-} lakini kitenzi kilichotumiwa ni cha Kiingereza. Ikiwa lengo la ukalimani ni kupitisha ujumbe kwa watu ambao hawaelewi lugha asilia basi lengo hili halitafanikiwa iwapo mkalimani atatumia lugha hiyo katika tafsiri yake. Hii ina maana kuwa mtu ambaye haelewi lugha asilia hatapata ujumbe uliokusudiwa.

3.1.3 KIWANGO CHA KILEKSIA

Leksia inaingiliana sana na maana lakini hata hivyo maana inayolengwa hapa ni katika kiwango cha neno moja. Hivyo tumeangalia matumizi ya msamiati katika tafsiri.

Tatizo kubwa tulilogundua hapa ni kuwa kuna uzoevu miongoni mwa wakalimani kuwasilisha baadhi ya leksia jinsi zilivyo katika ujumbe asilia bila ya kuzitafsiri, licha ya kwamba visawe vya leksia kama hizo vipo katika lugha pokezi.

Mfano 1:

UA: For those attending this Conference...

UT: Kwa wale wanaohudhuria Conference hii.

Neno 'Conference' lina kisawe chake katika Kiswahili ambalo ni warsha. Hivyo tafsiri bora ingekuwa,

Kwa wale wanaohudhuria warsha hii.

Mfano 2:

UA: You go to private hospitals...

UT: Unaenda katika hospitali za private...

badala ya,

Unaenda katika hospitali za kibinafsi...

Mfano 3:

UA: They are just green.

UT: Yamekuwa ni Green tu.

Tatizo hapa ni katika kutafsiri neno 'green' ambalo katika Kiswahili ni kijani kibichi. Hivyo tafsiri bora ingekuwa;

Yamekuwa Kijani Kibichi tu.

Kutokana na uchambuzi wa mahubiri tuliyorekodi tuligundua kuwa kuna baadhi ya leksia zilizoundwa bila kuzingatia utaratibu wa kuunda msamiati. Mfano:

UA: He sees eternity

UT: Anaona umilele.

Katika mfano huu neno 'eternity' limetafsiriwa kama umilele ambalo yamkini linatokana na neno milele. Milele ipo katika

kategoria ya vielezi. Hivyo kama umilele ni nomino yaelekea imeundwa kutokana na kielezi. Hata hivyo kwa kawaida nomino za Kiswahili huundwa kutokana na vitenzi na vivumishi. Tafsiri bora zaidi ingekuwa;

Anaona maisha ya milele.

Tatizo lingine linatokana na matumizi ya leksia kijumla ambazo haziafikiani na dhana halisi zinazorejelewa katika ujumbe asilia.

Mfano 1:

UA: She might have visited a gynaecologist

UT: Anaweza kuwa ametembelea daktari

Neno lililotumiwa kama tafsiri ya 'gynaecologist' ambalo ni daktari ni la kijumla sana kwani halifafanui maana halisi ya neno 'gynaecologist'. Kuna daktari wa aina mbalimbali kwa mfano wa macho, wa watoto na kadhalika. Tungetarajia mkalimani hapa afafanue zaidi daktari huyo kama ifuatavyo;

Anaweza kuwa ametembelea daktari
anayeshughulikia magonjwa ya wanawake.

Mfano 2:

UA: Look at the video industry

UT: Tazama katika viwanda

Neno viwanda lililotumika kama tafsiri ya 'video industry' ni la kijumla sana kwani kuna viwanda vya aina mbalimbali.

Tafsiri bora ingekuwa;

Tazama kiwanda cha filamu

Pia hutokea wakati ambapo leksia zinazotumiwa si sahihi

kimaana zikilinganishwa na leksia za ujumbe asilia.

Mfano 1:

UA: This message will determine your life.

UT: Ujumbe huu utasababisha maisha yako.

Neno utasababisha halitoi maana iliyokusudiwa katika ujumbe asilia kwani neno hili lina maana sawa na 'to cause' katika Kiingereza. Hivyo neno lililotumiwa si sahihi. Tafsiri sahihi ingekuwa;

Ujumbe huu utaamua maisha yako.

Mfano 2:

UA: You feel guilty

UT: Unajisikia una ugumu

Neno ugumu ambalo ni tafsiri ya 'guilty' halitoi maana sahihi ya neno hili. Tafsiri bora ingekuwa;

Unajisikia una hatia.

Tatizo lingine tulilogundua ni ile hali ya mkalimani kutapatapa anapoteua visawe vya kutumia katika kutafsiri. Katika hali kama hii neno moja linatafsiriwa kwa kutumia maneno mawili tofauti.

Mfano 1:

UA: It was their desire...

UT: Ilikuwa matumaini yao...

Mfano 2:

UA: That was their desire

UT: Hiiyo ndiyo ilikuwa nia yao.

Licha ya kuwa maneno matumaini na nia yana maana tofauti, yametumiwa kama tafsiri ya neno moja ambalo ni 'desire'. Ni maoni yetu kuwa neno nia linaafiki zaidi kama tafsiri ya 'desire' Hivyo tafsiri bora katika mfano wa kwanza ungekuwa;

Ilikuwa nia yao...

Tatizo lingine ni athari ya Sheng katika msamiati unaotumiwa na wakalimani. Katika utafiti wetu tulishuhudia matumizi ya maneno ambayo yametokana na lugha hii ya Sheng.

Mfano 1:

UA: Luoism has gone...

UT: Ujadhe umeenda...

Badala ya; Uluo umeenda...

Mfano 2:

UA: We have seen Kikuyus and Kalenjins live together in peace.

UT: Tumeona Wakikuyu na Wakale wakiishi pamoja kwa amani.

badala ya;

Tumeona Wakikuyu na Wakalengin wakiishi pamoja kwa amani.

Kulingana na mkalimani mmoja tatizo kubwa katika kiwango hiki ni kupata kisawe katika lugha pokezi hivi kwamba wakati mwingine kulazimika kuelezea jambo fulani badala ya kulitafsiri moja kwa moja. Hata hivyo ni maoni ya Glemet (1958:107) kuwa:

"Kitu kimoja lazima kiwekwe wazi kuanzia mwanzo: si jukumu la mkalimani kutoa kisawe kamili.

Kazi yake ni kurudia kwa lugha
nyingine yale yaliyosemwa katika
lugha asilia akitumia msamiati
ulioko."

(tafsiri yetu)

Anapendekeza kuwa iwapo hakuna msamiati mwafaka basi ni bora
zaidi kuelezea neno lenyewe. Anamalizia kwa kusema kuwa
ugumu wa neno halipaswi kuwa tatizo kwa mkalimani aliyehitimu.

3.1.4 KIWANGO CHA MAANA

Maana ni jambo muhimu katika kazi yoyote ile ya
tafsiri kwani ni kiini cha ujumbe. Iwapo maana katika tafsiri
itapotoka basi ujumbe uliokusudiwa hubadilika kabisa. Kiwango
hiki cha maana ni muhimu kwa sababu mojawapo ya nadharia
zinazotuongoza katika utafiti wetu ni nadharia ya tafsiri
maana. Katika kiwango hiki tumeangalia maana inayobebwa na
fungu la maneno au sentensi kwa ujumla tofauti na kiwango
cha leksia ambapo tumelenga maana inayobebwa na neno moja.

Tumeangalia maana kama inavyojitokeza katika tafsiri
ya misemo na jazanda.

Mfano 1:

UA: He looked at him with the inner eye.

UT: Alimwalia na macho ya ndani.

Katika tafsiri yake, mkalimani ametumia tafsiri ya moja kwa
moja na hivyo maana iliyokusudiwa katika ujumbe asilia
haujitokezi. Ameangalia maana ya matamshi haya kijuujuu bila

kuzingatia kuwa kuna maana ya ndani inayobebwa na ujumbe asilia. Ni maoni yetu kuwa tafsiri mwafaka ingekuwa,

Alimwangualia kwa jicho la upekuzi.

Wakalimani tuliowahoji walikiri kuwa wao hutatizika sana katika kutafsiri misemo na methali kutoka Kiingereza hadi Kiswahili. Mkalimani mmoja alituelezea kuhusu tukio moja ambapo alikuwa akitafsiri mahubiri ya mchungaji mmoja kutoka Amerika. Kulingana na mkalimani huyu, mchungaji huyo alitunia msembo ambao mkalimani huyo hakuelewa maana. Msembo huo ulikuwa,

UA: I took a French leave.

ambao ulitafsiriwa na mkalimani huyo kama,

UT: Nilichukua livu ya Kifaransa.

Kwa vile mchungaji huyo hakuelewa Kiswahili hakuwa na habari kuwa tafsiri iliyotolewa ilikuwa na makosa. Mkalimani huyu aliendelea kutuambia kuwa ni baadaye ndipo aliarifiwa na wenzake kuwa 'French leave' ina maana ya kuacha kazi bila rufusa. Ni wazi kutokana na mfano huo kuwa waliopokea tafsiri hiyo hawakupata maana iliyokusudiwa katika ujumbe asilia.

Larson (1984:17) anasema kuwa nahau inapotafsiriwa moja kwa moja kuna uwezekano mkubwa wa kupotoshwa kwa maana asilia. Anaendelea kusema kuwa maana ya nahau haifai kutafsiriwa kwa kuangalia maana ya kila neno

linalotumika kama tulivyoona hapo juu. Anasema,

"Lengo la mtafsiri sharti liwe
kuwasilisha katika lugha
pokezi ujumbe ulioko katika
lugha asilia."

(tafsiri yetu)

Vivyo hivyo asemavyo Shitemi (1990: 145),

"Maana inayopatikana katika
tukio la lugha likichambuliwa
kwa kuangalia leksia zake au
sarufi ni tofauti na ile
inayopatikana iwapo tukio
hili litaangaliwa Kisemantiki
katika muktadha maalum. Tukio
lililo na maana Kileksia na
Kisarufi linaweza kukosa kuwa
na maana Kisemantiki..."

Ni muhimu kwa mkalimani kuelewa maana inayolengwa na
mhubiri wa ujumbe asilia. Hata hivyo matumizi ya sentensi
zilizo na utata yanaweza kuwa kikwazo katika kueleweka kwa
ujumbe.

Mfano 1:

UA: My focus today is on young
men and women.

UT: Leo nitazungumzia kuhusu vijana
wa kiume na wanawake.

Katika mfano huu sentensi inayotoa ujumbe asilia ina utata
sawasawa na tafsiri inayotolewa. Tafsiri inatoa ujumbe kuwa
wanaolengwa ni vijana wa kiume na wanawake wote kwa ujumla.
Maana iliyokusudiwa katika ujumbe asilia inajumuisha vijana,

wanaume kwa wanawake, jambo ambalo halijitokezi vizuri kutokana na utata ulioko katika sentensi hiyo. Ili kuondoa utata huo na kuleta maana iliyokusudiwa tafsiri bora ingekuwa;

Leo nitazungumza kuhusu vijana,
wake kwa waume.

Mfano 2:

UA: The love of the word...

UT: Upendo wa ulimwengu...

Katika mfano huu vilevile kuna hali ya utata ambayo inasababisha hali ya kutatanisha katika kuelewa maana iliyokusudiwa.

Kutokana na muktadha tuligundua kuwa maana iliyokusudiwa hapa si hali ya kupenda ulimwengu mbali ni hali ya kupenda vitu vya ulimwengu huu. Kama ilivyo katika mfano wa kwanza, hali ya utata unajitokeza hata katika ujumbe asilia. Ili kuondoa hali hii ya utata, tafsiri bora ingekuwa,

Kupenda mambo ya ulimwengu...

Kuna wakati ambapo mkalimani hutoa tafsiri ambazo hudhoofisha na kuchujua maana asilia ya ujumbe. Matokeo ya jambo kama hili ni kuwa maana hubadilika kabisa.

Mfano;

UA: A strong Christian will never be shaken.

UT: Mkristo mwenye nguvu hawezi kutingisika.

Katika mfano huu ujumbe asilia unarejelea Mkristo aliye imara lakini katika tafsiri tunapata maana ya Mkristo aliye na nguvu za kimwili. Hivyo maana inayojitokeza katika tafsiri ni

tofauti kabisa na ile iliyo katika ujumbe asilia. Hivyo tafsiri bora ingekuwa;

Mkristo imara hawezi kutingisika.

Kwa kumalizia, Ali (1981:21) anaelezea umuhimu wa maana katika tafsiri. Anasema,

"Ni muhimu kwa mtafsiri kujua
na kuweza kutambua kuwa
maana hupatikana katika kifungu
cha maneno wala si kwa
kuangalia kila neno pekee yake."

TANBIHI

1. Katika Guenther, F. (1978) Meaning and Translation: Philosophical and Linguistic Approaches
Gerald Duckworth & Company Ltd. London.
(UK.9)
2. Katika Kapinga (1983) Sarufi maumbo ya Kiswahili Sanifu (UK.15)
3. Tafsiri ya "an exception rather than a rule."
4. Katika kazi yake Kiswahili Lugha ya Taifa (UK 59-60)

4.0 UTANGULIZI

Kuna baadhi ya matatizo ambayo hutokana na mambo yasiyo ya Kiisimu. Katika sura hii tumeangalia matatizo hayo ambayo mara nyingi husababishwa na hali ya mkalimani na kiwango chake cha kufahamu lugha mbili zinazohusika.

Matatizo tutakayoshughulikia katika sehemu hii yana uhusiano mkubwa na matatizo ya Kiisimu tuliyoshughulikia katika sura ya tatu. Ni maoni yetu kuwa matatizo yasiyo ya Kiisimu wakati mwingi huwa kiini cha matatizo ya Kiisimu.

4.1 MATATIZO MENGINE YASIYO YA KIISIMU

4.1.1 MAFUNZO KWA WAKALIMANI

Umilisi wa lugha zote mbili ni muhimu kuhakikisha kuwa kazi ya tafsiri inafanywa kwa njia bora. Ni muhimu kwa mkalimani kuwa na umilisi wa kutosha katika lugha mbili zinazohusika ili aweze kuelewa maana ya ujumbe asilia na kuupitisha ujumbe huo katika lugha pokezi. Ni muhimu pia kutambua kuwa kuna tofauti kubwa kati ya kufahamu na kuwa na umilisi katika lugha fulani. Asemavyo Frerk (1959: 364),

"Kufahamu tu lugha hauna umuhimu wowote katika kazi inayohusiana na kutafsiri..."

(tafsiri yetu)

Anaendelea kusema kuwa kazi ya wakalimani na watafsiri ambao hawajapata mafunzo. na kufuzu huweza kusababisha upotoshaji wa ujumbe asilia.

Kutokana na utafiti wetu tuligundua kuwa wakalimani wengi huwa hawajapata mafunzo yoyote kuhusu kazi hii. Nida (1947:62) anasisitiza umuhimu wa kupitia mafunzo fulani hasa akirejelea watafsiri wa Bibilia. Anaona jambo hili kama mojawapo ya matayarisho muhimu kabla ya kuanza kazi ya kutafsiri. Mojawapo ya mafunzo muhimu yanahusiana na matumizi ya lugha. Nida pia anasisitiza mafunzo ya Kiisimu ambayo humwezesha mtafsiri kukabiliana na matatizo ya Kiisimu. Kutokana na maoni haya ya Nida, baadhi ya matatizo ya Kiisimu tuliyozungumzia katika sura ya tatu yanaweza kuepukika iwapo wakalimani watapata mafunzo kuhusiana na kazi hii.

Kutokana na mahojiano na baadhi ya wakalimani, maoni yao ni kuwa hakuna haja ya kupitia mafunzo fulani ndipo mtu aweze kuwa mkalimani. Kulingana nao, wakalimani wanaotumika katika makanisa mengi kwa kawaida huchukuliwa tu miongoni mwa waumini au wachungaji katika kanisa linalohusika. Kutokana na maelezo haya ni wazi kuwa mtu yeyote anayeelewa lugha mbili zinazohusika anaweza kuwa mkalimani.

Hata hivyo Glemet (1958:117) ambaye ni mkalimani aliyefuzu hakubaliani na mawazo kuwa anachohitajika kufanya mkalimani ni kujifunza lugha tu. Anasema kuwa,

"Mkalimani aliye na matatizo ya
lugha hafai kukubalika. Sharti

aelewe kila kitu katika lugha
inayohusika na atoe ujumbe bila
upotoshaji wa maana."

(Tafsiri yetu)

Anaona kuwa haya ni mawazo yanayopotosha kwani kuna mengi zaidi ya hayo. Ni maoni yake kuwa mkalimani anahitaji mafunzo katika taaluma hii yatakayomwezesha kufasiri lugha kwa urahisi zaidi.

Kutokana na mahojiano na baadhi ya wakalimani, tulifikia uamuzi kuwa mengi ya matatizo yanayowakabili wakalimani wa mahubiri ya kidini yanatokana na kutopata mafunzo katika kazi hii. Licha ya kwamba ukalimani ni taaluma kama taaluma zinginezo kama vile ualimu, uhandisi, utibabu na mengineyo, mengi ya makanisa yamechukulia kazi hii hivi hivi bila kuipatia umuhimu inayostahili.

Wataalamu wengine wa tafsiri pia wanazungumzia kuhusu lugha mbili zinazohusika katika tafsiri. Kulingana na Larson (1984), vitu viwili ni muhimu kuhusiana na lugha mbili zinazohusika ili kutoa tafsiri nzuri;

- i) Kuelewa vilivyo lugha asilia.
- ii) Kumiliki vilivyo lugha pokezi

Waandishi wa Better Translation for Better Communication wanazungumzia kuhusu mafunzo katika taaluma ya tafsiri. Wanaainisha mafunzo aina mbili;

- i) ya chuoni
- ii) ya kibinafsi

Wanasema kuwa,

"Katika mkutano uliofanyika
Nairobi mwaka 1976, UNESCO
ilipendekeza kuwa tafsiri
ni taaluma inayojisimamia
hivyo inahitaji mafunzo
maalum" (UK.95)

(Tafsiri yetu)

Kutokana na maelezo haya kuna haja ya kuwepo kwa wakalimani waliofuzu mafunzo yanayohusiana na tafsiri.

4.1.2 UJUMBE MREFU

Hutokea wakati ambapo mhubiri anaweza kutoa ujumbe mrefu sana bila kumwachia nafasi mkalimani atoe tafsiri. Jambo hili hasa hutokea bila ya mhubiri wa ujumbe asilia kukusudia. Katika mahubiri ya kidini, tatizo hili wakati mwingine hutokana na mhubiri wa ujumbe asilia kuingiwa na utamu wa ujumbe anaotoa hivi kwamba hataki kukatiza ujumbe huo. Hali kama hii inaweza kumkanganya mkalimani anapotoa tafsiri ya ujumbe ule na matokeo mara nyingi huwa upotoshaji wa ujumbe.

Kulingana na wakalimani, jambo hili ni nadra ingawa hutokea. Maoni ya mkalimani mmoja ni kuwa uwasilishaji wa ujumbe mrefu vilivyo utategemea uwezo wa kukumbuka ya mkalimani. Iwapo uwezo wake wa kukumbuka ni wa juu basi bila shaka hatapata matatizo yoyote. Lakini iwapo uwezo huo ni wa chini kuna uwezekano mkubwa na upotoshaji wa ujumbe.

Hali hii inaweza kutatiza zaidi iwapo ujumbe asilia umetolewa kwa kutumia lugha changamano. Katika tukio kama hili, kuna uwezekano mkubwa wa mkalimani kutowasilisha ujumbe wote uliokuwepo katika ujumbe asilia.

Glemet (1958:116) anazungumzia kuhusu ujumbe mrefu hasa katika ukalimani wa kufuatisha. Anaona kuwa jambo hili laweza kuwa tatizo kwa mkalimani. Anasema,

"Tafsiri ya ujumbe mrefu
inawezekana tu iwapo
anayetafsiri ataweza kunukuu
maneno au fungu la maneno
muhimu yanayopitisha wazo
fulani kwa ufupi."

(tafsiri yetu)

Hata hivyo akimnukuu Cicero¹ anaendelea kusema kuwa ni vigumu kupata mtu aliye na kipawa cha kuweza kukumbuka maelezo marefu bila kuyanukuu kwa utaratibu fulani.

Ujumbe mrefu pia unaweza kusababisha kutoeleweka vyema kwa ujumbe. Hapa huenda mkalimani asielewe ujumbe asilia uliotolewa. Ni muhimu kutambua kuwa mkalimani ana majukumu mawili muhimu sana ya kuelewa ujumbe asilia na wakati huo huo kutafsiri ujumbe huo. Hivyo iwapo ujumbe ni mrefu sana basi huenda ukaleta matatizo. Hapa umuhimu wa kupumua ili kumwachia mkalimani nafasi ya kutafsiri unajitokeza.

Kutokana na ujumbe mrefu, mkalimani anaweza kukwama kabisa hivi kwamba asiweze kutoa tafsiri kabisa. Jambo hili hasa

hutokana na hali ya kuchanganyikiwa. Katika utafiti wetu tulishuhudia wakati mmoja ambapo mhubiri wa ujumbe asilia agunduapo kuwa ujumbe alioutoa ni mrefu sana aidha hurudia ujumbe huo au humsaidia mkalimani kutafsiri ujumbe huo.

Jambo lingine muhimu ni kiwango cha kutoa ujumbe asilia. Iwapo mhubiri atatoa ujumbe wake kwa kasi sana kuna uwezekano wa yale yanayotafsiriwa kutopokelewa vilivyo na waumini. Kwa mfano katika utafiti wetu tulishuhudia wakati ambapo mhubiri wa ujumbe asilia alikuwa akienda kwa kasi mno hivi kwamba anaanza ujumbe mwingine kabla ya mkalimani kumaliza kutoa tafsiri ya ujumbe uliotangulia. Matokeo yake ni kuwa ule ujumbe uliotafsiriwa haukuweza kueleweka kwani mkalimani alilazimika kuacha ujumbe nusu nusu ili aweze kumfikia mhubiri wa ujumbe asilia. Tukio kama hili linaweza kuwa kikwazo kwa uwasilishaji wa ujumbe katika lugha pokezi.

Eisler (1968:87) anasema kuwa mojawapo ya matatizo ambayo huzungumziwa na wakalimani waliohitimu yanahusiana na mwendo wa kasi. Hata hivyo Eisler akimnukuu Seleskovitch (1965) anasema kuwa;

"Kiwango cha maneno kwa
dakika hakipaswi kupita
maneno mia moja hamsini
na mkalimani huwa amefikia
kiwango hiki anapomaliza
mafunzo yake."

(tafsiri yetu)

4.1.3 HISIA ZA MKALIMANI

Hisia ni jambo ambalo huwa halijitokezi waziwazi lakini huweza kuathiri mkalimani katika kazi yake. Tafsiri anayotoa mkalimani itategemea vile anavyochukulia lugha mbili zinazohusika.

Kutokana na mahojiano na wengi wa wakalimani, maoni yao ni kuwa Kiingereza ni lugha iliyo na hadhi ikilinganishwa na Kiswahili. Hisia za wengi wao ni kuwa Kiswahili ni lugha rahisi inayoweza kutumiwa na yeyote anayeifahamu. Hata hivyo kwa maoni yetu Kiswahili walichokuwa wanakirejelea hapa ni kile Kiswahili cha mtaani² ambacho hutumiwa na watu wengi katika mazungumzo ya kawaida. Hivyo tatizo moja tulilogundua hapa ni hali ya kukuza lugha moja na kudunisha lugha nyingine kati ya lugha mbili zinazohusika katika tafsiri. Matokeo yake ni kuwa tafsiri inayotolewa kwa lugha iliyodunishwa huwa haizingatii usanifu wa lugha hiyo. Maoni yetu ni kuwa hisia kama hizi huweza kuchangia katika matatizo ya Kiisimu tuliyoangalia katika sura ya tatu.

Mahubiri ya kidini huweza kuwa na ujumbe unaoweza kuchoma roho za waumini wengi. Mapokezi ya ujumbe kama huu huwa tofauti kutegemea mada inayohusika. Hutokea wakati ambapo hisia za mhubiri wa ujumbe asilia hutofautiana na zile za mkalimani anayetafsiri ujumbe huo.

Maoni ya baadhi ya wakalimani kuhusiana na jambo hili

ni kuwa kuna baadhi ya wahubiri ambao wana tabia ya kushambulia kundi fulani miongoni mwa waumini, jambo ambalo huweza kuleta madhara makubwa. Katika hali kama hii mkalimani huona ana jukumu la kujaribu kufunika au kuyaacha baadhi ya mambo katika ujumbe asilia. Matokeo yake ni kuwa ujumbe uliotafsiriwa huwa tofauti kabisa na ule ujumbe asilia. Madai ya mmoja wa wakalimani ni kuwa mkalimani anapofanya hivyo huwa katika hali ya kuzingatia masilahi ya waumini.

Wakalimani wengine wana maoni tofauti. Kwao wanasisitiza umuhimu wa kutoa tafsiri ya ujumbe asilia kwa uaminifu bila kubadilisha au kuacha jambo lolote. Maoni yao kuhusu wakalimani ambao hujaribu kubadilisha ujumbe asilia ni kuwa wao hufanya hivyo kwa sababu za kibinafsi. Mkalimani mmoja anatupa mfano ambapo msimamo wa kisiasa wa mhubiri wa ujumbe asilia na wa mkalimani unatofautiana. Katika hali kama hii kuna uwezekano wa mkalimani kubadilisha ujumbe kulingana na msimamo wake. Wakati mwingine wakalimani huweza kutumia mbinu hii kuwavuta wasikilizaji.

Wanaopinga jambo hili la kubadilisha ujumbe asilia wanaona kuwa hisia kama hizi za kibinafsi katika ukalimani huweza kuleta madhara makubwa katika ujumbe unaowasilishwa kwa waumini. Matokeo yake ni kuwa mahubiri hukosa maana. Kundi hili la wakalimani wanashutumu hasa wakalimani wanaotafsiri mahubiri njiani kwa kutumia taaluma hii kama mbinu ya kuwavutia wapita njia hivi kwamba wengi wao huwa hawatambui umuhimu wa ukalimani katika mahubiri ya kidini.

Licha ya haya yote wengi wa wakalimani wanakiri kuwa hisia za kibinafsi zinaweza kuwa kikwazo katika uwasilishaji wa ujumbe.

4.1.4 SAIKOLOJIA YA MKALIMANI

Uwezo wa kukumbuka huhusishwa na saikolojia ya binadamu. Hivyo iwapo mkalimani hana uwezo mzuri wa kukumbuka basi atakabiliwa na matatizo mengi hivyo kumlazimu mhubiri anayetoa ujumbe asilia kurudiarudia ujumbe huo mara kwa mara. Kutokana na uchunguzi wetu tuligundua kuwa jambo hili laweza kusababisha hali ya uchovu miongoni mwa waumini hivyo kuathiri upokeaji wa ujumbe. Katika utafiti wetu tuligundua kuwa hali kama hii wakati mwingine humlazimu mhubiri wa ujumbe asilia kumsaidia mkalimani kutafsiri ujumbe huo. Matokeo yake ni kuwa kunakosekana mtiririko katika ujumbe unaotolewa.

Seleskovitch (1984)³ anasema kuwa ni muhimu kutilia maanani yale ambayo hufanyika ubongoni mwa mtafsiri hasa wakati wa kitendo cha tafsiri. Ni maoni yake kuwa tafsiri ipo kati ya mambo ya Kiisimu na kisaikolojia.

Muhimu pia ni uwezo wa mkalimani wa kujieleza. Kuna uwezekano mkubwa wa mkalimani kuelewa ujumbe asilia lakini akashindwa kupata maneno mwafaka ya kujieleza katika lugha pokezi. Katika hali ya kujaribu kujieleza hutokea matatizo kama vile kuteleza kwa ulimi.

Crystal (1987:262) anaeleza kuteleza kwa ulimi kama,

"...kugeuza bila kukusudia
yale yaliyonuiwa kusemwa
na mzungumzaji..."

(tafsiri yetu)

Sigmund Freud⁴ aliona kuteleza kwa ulimi kama ishara ya nguvu zisizofahamika au kuchanganyikiwa kwa akili miongoni mwa watu wanaohusika. Ingawa hatukuweza kukumbana na tatizo hili katika utafiti wetu, hili ni tatizo ambalo huwatatiza watu wengi katika mazungumzo, wakalimani wakiwemo.

Ni muhimu kwa mkalimani kuwa na uwezo wa kuelewa ujumbe ulioko katika lugha asilia. Iwapo mkalimani hakuelewa vilivyo ujumbe katika lugha asilia basi atapata matatizo kuwasilisha ujumbe huo katika lugha pokezi. Kukosa kuelewa ujumbe huweza kusababishwa na kutosikia vizuri ujumbe asilia. Aitchison⁵ anaeleza kuwa kutosikia hudhihirisha kuingizwa kwa leksia mahali ambapo sehemu ya ujumbe haukusikika vizuri. Katika utafiti wetu, tuligundua kuwa tatizo hili linaweza kutokea pale ambapo maneno yanayohusika yanakaribiana hasa kimatamshi.

Pamoja na hayo mkalimani huwa na jukumu la kuchanganua ujumbe asilia akilini mwake kabla hajautafsiri. Kulingana Poisson (1975)⁶, tafsiri inayofanywa na binadamu ni kazi iliyo na mahitaji mengi. Baadhi ya mambo anayotaja ni kama vile ujuzi wa kujieleza, uwezo wa kuchanganua ujumbe asilia na uwezo wa kukumbuka.

Kuna baadhi ya matatizo ambayo huwa si muhimu sana lakini yamkini mkalimani hujua kuwa yapo na yanaweza kutatiza uwasilishaji wa ujumbe.

Kutokuwa na tajriba katika kazi hii huweza kuwa tatizo. Kuna ule uoga unaoweza kumshika mtu anapokuwa jukwaani. Uoga jukwaani hutokea hasa wakati mzungumzaji hawezi kubashiri vile wasikilizaji wake wanavyompokea. Matokeo yake ni hali ya kuwa na uoga na kuchanganyikiwa. Haya ni mambo ambayo hufanyika ndani, lakini asemavyo Eisenson (1963) huweza kujitokeza nje kupitia sauti inayotetemeka, hali ya kusitasita, vitendo visivyohitajika na hali ya kutokuwa na udhabiti kwa ujumla. Anaendelea kusema akimnukuu Knisley (1951)⁷ kuwa tatizo hili huweza kuwakabili hata wazungumzaji walio na tajriba wakati mmoja au nyingine. Tofauti ni kuwa mzungumzaji aliye na tajriba huweza kujituliza kwa haraka akilinganishwa na yule ambaye hana tajriba.

Mkalimani mmoja anatueleza vile alivyokuwa na wakati mgumu alipoteuliwa kufanya kazi hii ya ukalimani kwa mara ya kwanza. Alikuwa na hofu kama tafsiri aliyotoa ilikuwa sawa. Alikabiliwa na hali ya kusitasita kwani hakuwa na imani na yale aliyokuwa anayasema.

Kulingana na wengi wa wakalimani, tatizo lingine linaweza kusababishwa na uchovu. Maoni yao ni kuwa kazi hii inahitaji kujitayarisha kiakili na kimwili. Wakalimani wengi tuliowahoji huwa na kazi zingine wanazofanya mbali na kazi hii ya ukalimani. Wengi wao hukabiliwa na tatizo hili wanapotarajiwa kufanya kazi hii ya ukalimani katika ibada za jioni. Katika wakati kama huu wao huwa wamechoka hivi kwamba hawawezi kufikiria vizuri.

Mkalimani mwingine tuliyemhoji anasema kuwa jambo hili pia laweza kuwa tatizo wakati wa mikutano ya Injili ambapo

wanahitajika kusafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine. Anasema kuwa hutokea wakati ambapo wao hufika katika mikutano wakiwa wamechelewa hivi kwamba hawapati nafasi ya kupumzika.

Kutokana na uchunguzi wetu tuligundua kuwa wakalimani wa mahubiri ya kidini hufanya kazi hii kama kazi ya kujitolea. Hii ina maana kuwa hawatarajii malipo yoyote.

TANBIHI

1. Cicero alikuwa mwanafalsafa mashuhuri wa Kiurumi.
2. Kiswahili kisicho sanifu.
3. Kulingana na Namulungu (1997)
4. Katika The Cambridge Encyclopedia of Language (1987:262)
5. Katika An Encyclopedia of Language (1990:331)
6. Katika Better Translation for Better Communication (1983:99)
7. Katika kitabu chake An Investigation of the Phenomenon of Stage Fright in certain Prominent Speakers. (UK. 124-125)

5.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Kutokana na utafiti wetu tumegundua kuwa matatizo ya kiisimu yanatokana na uzoevu wa kutumia lugha ambayo sio sanifu katika mazungumzo. Ukalimani ambao huwasilishwa katika lugha zungumzi hivyo umeathiriwa na matumizi haya. Matatizo haya pia husababishwa na athari ya lugha ya kwanza hasa katika kiwango cha fonolojia na sintaksia. Katika kiwango cha leksia na maana matatizo hasa hutokana na kutofahamu vilivyo lugha mbili zinazohusika katika tafsiri.

Kwa upande wa matatizo yasiyo ya kiisimu, tumegundua kuwa matatizo haya huchangia katika matatizo ya kiisimu. Kwa mfano kutokana na uchunguzi wetu tulipata kugundua kuwa wakalimani waliopata mafunzo kuhusiana na kazi hii hutumia lugha kwa ufasaha zaidi wakilinganishwa na wale ambao hawajapata mafunzo yoyote. Hivyo ni maoni yetu kuwa matatizo yasiyo ya kiisimu sharti yachunguzwe ili kutatua matatizo ya kiisimu.

Uchunguzi wetu umeongozwa na haipotesia mbili ambazo zimeweza kupimwa. Kutokana na utafiti wetu tumeweza kuthibitisha kuwa kwa kiwango fulani ujumbe mrefu unaweza kuwa tatizo kwa mkalimani, japo si kila wakati. Vilevile katika haipotesia yetu ya pili tumeweza kuthibitisha kuwa baadhi ya makosa yanayojitokeza katika ujumbe asilia humulikwa katika fasiri yake. Hata hivyo ni maoni yetu kuwa kuna uwezekano mkubwa wa kuwa na tafsiri bora kuliko ujumbe asilia.

Kutokana na utafiti wetu, ni wazi kuwa wakalimani wengi wa mahubiri ya kidini huwa hawajapitia mafunzo yoyote kuhusiana na kazi hii. Kati ya wakalimani kumi tulioweza kuwahoji ni wawili pekee waliopata mafunzo kuhusu tafsiri. Kutokana na hojaji tulizoweza kukusanya hakuna hata mkalimani mmoja aliyepata mafunzo kuhusu tafsiri. Kwa maoni yetu, jambo hili ni kikwazo kikubwa katika taaluma hii. Licha ya kuwepo kwa shule zinazotoa mafunzo kuhusu tafsiri, utafiti wetu ulidhihirisha kuwa ni wakalimani wachache mno ambao hupitia mafunzo hayo. Hivyo tunakubaliana na Shitemi (1990:168) anaposema kuwa watafsiri wengi si wataalam wa somo tafsiri. Katika utafiti wetu tuligundua kuwa wakalimani wengi huteuliwa tu miongoni mwa waumini au wachungaji. Maoni yetu ni kuwa wakalimani wa mahubiri ya kidini wanahitaji kupewa mafunzo katika kazi hii kama wakalimani wenzao katika mikutano ya kimataifa.

Kwa maoni yetu, ukalimani haujapewa umuhimu unaostahili hasa miongoni mwa madhehebu mbalimbali ya kidini. Mwelekeo huu ni sharti ubadilike iwapo tunatarajia kupata kazi bora ya ukalimani.

Udhaifu katika kazi ya ukalimani pia unatokana na sababu kuwa mkalimani huwa hana fursa ya kupitia kazi yake kabla ya kuwasilisha. Licha ya kuwa hili ni jambo ambalo haliwezi kuepukika katika muktadha wa kazi hii, ni muhimu iwapo mkalimani atadokezewa mada itakayozungunziwa na mhubiri wa ujumbe asilia ili aweze kujiandaa.

Kwa kumalizia, maoni yetu ni kuwa kuna haja ya kufanywa uchunguzi zaidi katika uwanja huu wa ukalimani. Kazi yetu imeshughulikia ukalimani wa kufuatisha tu ambao hutumika katika mahubiri ya kidini. Kuna ukalimani sawia ambao hatukuuangalia

kwa undani. Hivyo utafiti zaidi bado unahitajika.

Achilles, (1971) 'Some Reflections on the Difficulty of Translation' Katika Wright, A. (ed) Studies in Chinese Thought, University of Chicago Press, Chicago.

Ala C.W. (1981) 'The Problems of Translating from English into Kiswahili: As Exemplified by V.G.E News Items.' Tanzania ya M.A., U.O.M.

Barrett, A. (1974) Translating the Word of God? Zondervan Publishing House, Grand Rapids Michigan.

Barrett, A. (1972) Discourse Analysis, Cambridge University Press, U.S.A.

Barrett, A. (1965) A Linguistic Theory of Translation, U.U.P., London.

Barrett, A. (ed) (1990) An Encyclopedia of Language, Routledge, London.

Barrett, A. (1987) The Cambridge Encyclopedia of Language, Cambridge University Press, Australia.

Barrett, A. (1983) The Psychology of Communication, Meredith Publishing Company, New York.

MAREJELEO

- Achilles, F. (1967) 'Some Reflections on the Difficulty of Translation' Katika Wright, A. (ed) Studies in Chinese Thought University of Chicago Press, Chicago.
- Ali, C.W. (1981) 'The Problems of Translating from English into Kiswahili: As Exemplified by V.O.K News Items.' Tasnifu ya M.A., U.O.N.
- Beekman, J. na Callow, J. (1974) Translating the Word of God; Zondervan Publishing House, Grand Rapids Michigan.
- Brown, G. na Yule, G. (1983) Discourse Analysis; Cambridge University Press, U.S.A.
- Catford J.C. (1965) A Linguistic Theory of Translation; O.U.P, London.
- Collinge I.N. (ed) (1990) An Encyclopedia of Language; Routledge, London.
- Crystal, D. (1987) The Cambridge Encyclopedia of Language; Cambridge University Press, Australia.
- Eisenson, J. (1983) The Psychology of Communication; Meredith Publishing Company, New York.

- Eisler, F. (1968) Psycholinguistics; Academic Press, London.
- Frerk, C.W. (1959) 'Training of Translators' katika Cary & Jumplet (ed) of Quality in Translation; Pergamon Press, Paris.
- Fuller, F. (1984) The Translator's Handbook, Gerrard Cross, Buckinghamshire.
- Gleimet, R. (1958) 'Conference Interpreting' katika Aspects of Translation University of London Communication Research Centre.
- Guethner, F. et al (1978) Meaning and Translation: Philosophical and Linguistic Approches; Gerald Duckworth and Co. Ltd, London.
- Hartmann, R.R.K. na Stork, F.C. (1972) Dictionary of Language and Linguistics; Applied Science Pub. Ltd, London.
- Larson M. L. (1984) Meaning Based Translations: A Guide to Cross Language Equivalence; University Press of America.
- Macdonell D. (1986) Theories of Discourse Basil Blackwell Ltd. UK.
- Makay, J. (1973) Exploration in Speech Communication; Charles E. Merrill Publishing Company Columbus.

- Mutie, E.K. (1997) 'Sanaa katika Tafsiri: Matatizo na Athari zake' Tasnifu ya M:A., U.O.N.
- Namulungu, R.I.S. (1997) 'Ukiushi katika Tafsiri: Uhakiki wa Shamba la Wanyama', Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret.
- Newmark, P. (1988) A Textbook of Translation: Prentice Hall International, UK. Ltd.
- Nida, E. (1947) Bible Translating; America Bible Society, New York.
- _____ (1964) 'Linguistic and Ethnology in Translation Problems' katika Hymes, D. (ed) Language in Culture and Society. Harper and Row Publishers.
- Omondi, F.O. (1997) 'Dhana na matatizo ya Tafsiri: Tathmini ya Risasi Zianzapo Kuchanua' Tasnifu ya M:A., U.O.N.
- Pei, M. na Gaynor, F. (1969) A Dictionary of Linguistics New Jersey; Littlefield, Adams & Co. Totowa.
- Shitemi N.L. (1990) 'Mawasiliano katika Tafsiri: Uteuzi wa Mtafsiri' Tasnifu ya M.A., U.O.N.

TUKI (1981)

Kamusi ya Kiswahili Sanifu;
O.U.P., Dar-es-Salaam.

_____ (1990)

Kamusi Sanifu ya Isimu
na Lugha; Educational
Publishing and Distributors
Ltd. Dar-es-Salaam.

Van Dijk, B.M. (1983)

Better Translation for
Better Communication;
Pergamon Press, Oxford.

Zaja, J.O. (1986)

'Fasihi Tafsiri Katika
Ukuzaji wa Fasihi ya
Kiswahili: Matatizo na
Athari zake.' Tasnifu
ya M.A., U.O.N.